

UJUMBE KAMILIFU

Unacho stahili kufahamu


Toleo la 1

Vyanzo vya habari kuhusu COVID-19

- [MyAus COVID-19 App](#) ni programu iliyoendelezwa na baraza la uhamiaji wa Australia, inayotoa habari kuhusu COVID-19 na msaada katika lugha 24 za jamii. Unaweza kuipakua kutoka App Store au Google Play.
- www.coronavirus.nt.gov.au ni tovuti ya serikali ya Wilaya ya Kaskazini inayo ujumbe kuhusu kanuni za afya, ncha za usalama, udhibiti wa mipaka na maeneo tajika.
- Rasilimali mbalimbali za kutafsiriwa pia zinapatikana katika tovuti za serikali ya Australia [Department of Health website](#)
- [COVIDSafe App](#) ni programu iliyoendelezwa na serikali ya Australia na inatumika kuongeza kasi katika kuwafuatilia walio wazi kwa maambukizi ya COVID-19. Unaweza kuipata kutoka App Store au Google Play.

Jikinge mwenyewe pamoja na wengine

- Kaa kwa umbali wa mita 1.5 kando na mwenzio.
- Zuia kusalimiana kwa mikono unapokutana na watu.
- Usiwakumbatie au kuwabusu watu nje ya familia unayoishi nayo.
- Osha mikono yako kwa sabuni na maji na kutumia “hand sanitiser” mara kwa mara.
- Kohoa na piga chafya unani mwa kiwiko chako au tumia tishu na kuitupa mara moja.
- Iwapo unahisi kuwa mgonjwa, jitenge na wengine na umpigie daktari au piga nambari ya dharura ya COVID-19 katika wilaya ya kaskazini, 1800 008 002.



Watu wanaokuja katika wilaya

Iwapo una jamaa na marafiki wanaopanga kuja katika Wilaya ya Kaskazini, watahitaji:

- Kujaza fomu ya kuingia mpakani, bila kujali watokapo. Tembelea www.coronavirus.nt.gov.au kujaza fomu hiyo.
 - Watu wanaowasili katika Wilaya ya Kaskazini na wamekuwa katika maeneo tajika ya COVID-19 kwa siku 14 zilizopita watahitajika:
 - Kuenda katika karantini ya lazima na inayosimamiwa kwa siku 14 kwa gharama yao wenyewe.
 - Gharama kwa kila mtu ya karantini ya lazima na inayosimamiwa ni \$2,500
- Taarifa muhimu – karantini inayosimamiwa**
- Watu katika karantini ya kusimamiwa watahitaji kupimwa kabla ya kutoka kwenye karantini.
 - Iwapo watakata kupimwa, kutakuwepo na siku 10 zaidi zitakazoongezwa katika muda wa karantini.

- Watakaopatikana kupeana taarifa ya kupotosha katika fomu ya kuwasili wataweza kupokea faini ya \$5,056 kwa mtu binafsil, \$25,280 kwa biashara na uwezekano wa muda gerezani isiyozidi miaka mitatu.

Maeneo tajika ya COVID-19 ni nini?

Maeneo tajika ni yale maeneo katika Australia ambapo wingi wa maambukizi mapya ya COVID-19 yamerekodiwa, na yametangazwa na Afisa Mkuu wa Afya katika Wilaya ya Kasakazini. Maeneo tajika yameorodheshwa kisheria ili watu wanaoingia Wilaya ya Kaskazini kutoka maeneo hayo tajika wanaweza kutambulika. Orodha ya maeneo tajika inaweza patikana kwenye tovuti, [COVID-19 website](#).

- Hakuna msamaha wa usafiri utakaopewa kwa watu kutoka maeneo tajika
- Kila mtu anahitaji kufahamu maeneo tajika yalipo.
- Maeneo haya yanaweza badilika kwa haraka, kwa hivyo ni muhimu uwe na ujumbe kamili.

Yeyote anayeishi au ametembelea eneo tajika hataruhusiwa kuzuru Wilaya ya Kaskazini.

Matukio na mikusanyiko

Kuna mahitaji mbalimbali kulingana na ukubwa wa tukio lako.

- **Idadi ya watu chini ya 100**

Mikusanyiko yenye idadi chini ya watu 100 haihitaji orodha au mpango wa usalama. Kujiweka mbali kimwili na watu pamoja na usafi lazima uzingatiwe.

- **Idadi ya watu 100 hadi 500**

Matukio n mikusanyiko ya watu 100 hadi 500 lazima yahakikishe orodha ya usalama wa COVID-19, [COVID-19 safety checklist](#). Kujiweka mbali kimwili na watu pamoja na usafi lazima uzingatiwe.

- **Idadi ya watu zaidi ya 500**

Matukio na mikusanyiko ya umma ya watu zaidi ya 500 lazima yahakikishe orodha ya usalama wa COVID-19, [COVID-19 safety checklist](#). Kujiweka mbali kimwili na watu pamoja na usafi lazima uzingatiwe.

Dalili na Hatari za COVID-19

COVID-19 ni ugonjwa wa kupumua unaosababishwa na virusi vipya. Dalili ni kama joto jingi, kukohoa, maumivu kwenye koo na upungufu wa pumzi. Virusi hivi vinaweza kusambaa kutoka kwa mmoja hadi mwingine kwa urahisi. Kwa sasa hakuna chanjo au tiba ya COVID-19.

Watu wenye uwezekano wa kuwa katika hatari kubwa ya kuwa wagonjwa wakiambukizwa virusi hivi ni:

- Kila mtu mgonjwa na ana hali sugu ya kiafya au kinga hafifu ya mwili.
- Watu wenye umri wa miaka 70 na zaidi
- Watu asili (Aboriginal) na wale wa kisiwa cha Torres Strait wenye umri wa miaka 50 na zaidi, na wenye hali mbaya ya kiafya moja au zaidi.

